**HOTUBA YA MHE. DKT. SALIM AHMED SALIM WAZIRI MKUU MSTAAFU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA KONGAMANO LA UMOJA WA VIJANA WA CCM LA KUMKUMBUKA MWALIMU NYERERE TAREHE 14 OKTOBA 2010 KATIKA UKUMBI WA KARIMJEE, DARE ES SALAAM.**

## SHUKURANI

Napenda kutanguliza Shukurani na hongera kwa Umoja wa Vijana wa CCM kwa kuandaa kongamanoo hili. Kongamano hili ni zaidi ya kumkumbuka Mwalimu Nyerere. Ni kongamano la kujifunza na kukumbushana umuhimu na wajibu wa kuzingatia yale mambo ya msingi aliyoyasimamia kama muasisi wa Taifa letu na kiongozi wetu.

## UTANGULIZI

Tarehe 14 Oktoba mwaka huu tunatimiza miaka 11 tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere aiyage dunia mwaka 1999. Tangu wakati huo, Watanzania tumejiwekea utaratibu wa kuitumia tarehe hiyo kumkumbuka na kumuenzi Mwalimu kwa kwa mchango wake mkubwa kwa Tanzania, Afrika na dunia kwa jumla na hasa wananchi wa dunia ya tatu.

Kifo cha Mwalimu Nyerere kilikuwa pigo kubwa sio tu kwa watanzania bali pia kwa Afrika na wapenda haki na usawa duniani kote. Kifo hicho kilihuzunisha na kufaidhisha wengi barani Afrika na sehemu mbalimbali za dunia.

## MWALIMU ANAVYOTAMBULIKA DUNIANI KOTE:

Mwalimu Nyerere anatambulika kama kiongozi aliyejipatia sifa kubwa yeye mwenyewe na taifa letu. Alikuwa ni kiongozi ambaye aliamini na alichukua hatua

kwa nguvu zake zote kuhakikisha anajenga na kulinda uhuru, umoja, utu, haki, amani na utulivu.

Pamoja na kuwa Rais wetu wa kwanza, Mwalimu anakumbukwa kama miongoni mwa viongozi thabiti ambaye aliongoza vuguvugu la ukombazi wa taifa letu kutoka katika makucha ya ukoloni. Aliamini na kuhakikisha kuwa watanzania wanapaswa kuwa huru na kujiendeshea mambo yao wenyewe katika misingi waliyojiwekea wenyewe.

Mwalimu Nyerere aliamini katika utu na alitumia maisha yake yote kusisitiza umuhimu wa kuthamini utu wa mtu yeyote yule hata kama mnatofautiana naye kifikira, kielimu, kiimani, kipato na tofauti zingine zozote. Ndio maana pamoja na viongozi wenzie waasisi wa taifa letu walikubaliana kuwa binadamu wote ni sawa kama imani ya kwanza ya wanachama wa TANU na baadaye CCM.

Katika misingi hiyo ya utu, Mwalimu alijali maisha ya watu wake kwa hali na mali. Katika kujali huko aliweza kutambua mapema na kutangaza vita dhidi ya maadui watatu wakubwa ambao ni umasikini, maradhi na ujinga. Kwa ustadi wa hali ya juu, Mwalimu alitambua umuhimu wa kupigania uhuru sio wa Tanzania tu lakini wa bara letu lote, kujenga umoja, mshikamano na udugu miongoni mwetu kama silaha madhubuti za kupambana na maadui hao.

Ndio maana alisimama kidete kupinga njama na au vitendo vyotevyote vile vilivyokuwa vinaashiria kuvunja umoja na mshikamano wa taifa letu. Alielewa na kuamini kuwa Tanzania ni ya watu wote wenye makabila, rangi na dini tofauti. Daima alikemea kwa nguvu zake zote chochote kile kilicholenga kuleta mfarakano. Alikuwa

ni kiongozi asiyekuwa na mzaha kwa kitendo ama neno lolote lile la kutaka kuwagawa watanzania.

Mwalimu Nyerere aliamini katika kuhakikisha kuwa haki inatendeka na alitambua kuwa bila ya haki hakutakuwa na amani na utulivu na hivyo hakutakuwa na uwezekano wa kupiga vita majanga ya umasikini, ujinga na maradhi kama alivyodhamiria.

Kama yeye mwenyewe alivyosisitiza kwenye Mkutano Mkuu wa CCM tarehe 22/10/1987. Na hapa nanukuu;

> *"Umoja na Amani ni nguvu kubwa duniani. Ni nguvu kubwa kwa mataifa madogo na makubwa. Kwa nchi changa na maskini kama yetu, umoja na amani ni Amana na Tunu kubwa isiyo na bei.......Tukiulizwa na wenye kiburi na fidhuli ya wingi wa mali: Mna nini ninyi Watanzania? Tunaweza kujibu si kwa fidhuli lakini kwa fahara kabisa: tuna Umoja na Amani; vitu ambavyo havinunuliki kwa kiasi chochote cha fedha. Tuna haki kujivunia Umoja huu na Amani hii maana ndivyo vilivyotuwezesha kupambana na matatizo makubwa ya vita, ya uchumi na hata ya kisiasa. Tuna haki ya kujivuna kwa sababu Umoja huu na Amani hii havikuzuka vyenyewe tu: mbona havizuki kila mahali? Wahenga wanasema; "ukiona vinaelea vimeundwa."*

Mwalimu Nyerere anaendelea kueleza kuwa "Msingi wa Amani ni Haki. Ama Haki yenyewe kama ipo, na matumaini ya kujenga Taifa lenye haki. Panapokuwa hapana Haki wala Imani na Matumaini ya kupata Haki, hapawezi kuwa na Amani na utulivu wa kiasiasa. Hatima yake patazuka fujo, utengano na mapambano. Mwalimu

anasema "Tumeweza kujenga Umoja na Amani katika nchi yetu, siyo kwa sababu tumefaulu kujenga Taifa lenye haki, bali kwa sababu wananchi wa Tanzania wameendelea kuwa na imani ya kujenga jamii yenye haki na usawa".

**Ndugu Viongozi na Ndugu Washiriki wa Kongamano,**

Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi mwadilifu kwa dhamira na matendo yake. Daima aliishi maisha ya mfano wa uadilifu na kuhakikisha kuwa anajenga maadili ya uongozi ambayo yanasisitiza uadilifu. Alichukia rushwa kwa vitendo na kamwe hakumuonea aibu mtu yeyote ambaye alihusika katika kutoa ama kupokea rushwa. Ndio maana tunaona kuwa katiba ya Chama Cha Mapinduzi inazungumzia kuwa rushwa ni adui wa haki. Mwanachama wa CCM anakula kiapo cha kutotoa wala kupokea rushwa.

Mwalimu alikuwa mstari wa mbele katika kusimamia yale aliyoyaamini. Mojawapo ni lile la Itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea. Mwalimu aliamini kwa dhati kabisa kuwa sera za Ujamaa na Kujitegemea ndizo zingeliweza kujenga jamii isiyokuwa na tofauti kubwa kati ya walio nacho na wasio nacho. Hata hivyo wakati alikuwa na msimamo usiotetereka katika kusimamia hayo anayoyaamini lakini pia alikuwa si mbishi wa kukubali mabadiliko pale ambapo anajithibitishia kuwa ni mabadiliko sahihi ama yasiyo epukika.

Kwa kifupi Mwalimu Nyerere alijenga misingi na maadili ambayo yalitufanya sote tujivunie Utanzania wetu ndani na nje ya nchi. Alikuwa kiongozi aliyeamini kwa dhati kuwa kiongozi mzuri ni yule anayeenziwa na watu wake wakati akiwa madarakani lakini pia akiwa hayupo madarakani. Mwalimu hakuwa malaika na wala hakukosa

mapungufu yake. Lakini pale alipogundua makosa yake hakusita kukiri na kubadilika.

## MWALIMU NA AFRIKA

Mwalimu Nyerere anakumbukwa kote barani Afrika kama kiongozi ambaye aliyetambua kwamba uhuru wa nchi yake tu hautoshi bila ya uhuru wa nchi nyingine za kiafrika. Alitambua pia kuwa uhuru huo wa Tanzania usipokwenda sambamba na ukombozi wa nchi nyingine za kiafrika hatimaye utapata misukosuko mikubwa. Na kufuatia imani yake hiyo Mwalimu alisimama kidete kusaidia na kusimamia ukombozi wa bara la Afrika.

Kama alivyokuwa mwenzake Rais Kwame Nkurumah wa Ghana, Mwalimu alikuwa mstari wa mbele wa kupigania uhuru wa bara letu na umoja wa mshikamano wa Afrika kwa ujumla. Chini ya uongozi wake, Tanzania ilikuwa kama makao makuu ya mapambano dhidi ya ukoloni na ubaguzi wa rangi. Takriban viongozi wengi mnaowaona hivi sasa walikuja hapa. Hapa ndio ilikuwa kama Mecca ya wapigania uhuru barani Afrika na hasa wale wa kusini mwa Afrika. Nchi yetu ilitoa mchango wa hali na mali kufanikisha lengo hilo. Itakumbukwa kwamba kwa kutambua mchango muhimu wa Tanzania katika ukombozi, Umoja wa Afrika OAU ulipoasisiwa mwaka 1963, miongoni mwa hatua zilizochukuliwa bila ya kusita ni kuunda Kamati ya Ukombozi (OAU Liberation Committee) na kuifanya Tanzania kuwa makao makuu yake.

Wale waliokuwa hawana upeo wa mbali walibeza msimamo huo wa Tanzania chini ya uongozi wa Mwalimu. Wapo wengine walikuwa wakimtuhumu Mwalimu kwa kujihusisha sana na suala la ukombozi na kudai kuwa kazi ya ukombozi wa mataifa

mengine haituhusu. Yeye aliamini kuwa uhuru wetu hauwezi kukamilika madhali majirani zetu kama Msumbiji, Zimbabwe, Namibia, Angola na sehemu nyingine za Afrika hawana uhuru. Lakini historia ilionyesha uthabiti wa msimamo wake huo. Mwalimu alifariki bara letu la Afrika likiwa huru ukiacha tatizo la Sahara Magharibi.

Hata baada a kustaafu kwake katika uongozi wa nchi na chama, Mwalimu alikuwa akifuatilia kwa ukaribu sana mambo ya Afrika na dunia ya tatu kwa ujumla.

Kwa mfano, wakati nikiwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Nchi za Afrika (OAU), nakumbuka wakati nilipomtembelea London akiwa mgonjwa sana mnamo mwezi Septemba mwaka 1999. Ingawa alikuwa kitandani na kusema kweli alikuwa mahututi, Mwalimu alisisitiza kwa hamu kubwa nimueleze masuala ya mkutano wa Sirte huko Libya ambapo Viongozi wakuu wa Afrika walikutana kujadii kuundwa Umoja wa Afrika (AU) kama hatua ya kuimarisha umoja uliokuwa wa OAU na kutanua Nyanja za ushirikiano na mshikamano. Pia Mwalimu katika mazungumzo yetu siku hiyo alionyesha dhahiri kuwa na shauku kubwa ya kurejea nyumbani haraka iwezekanavyo ili aendelee kusaidia kutatua mgogoro wa Burundi.

## MAZINGIRA NA CHANGAMOTO ZILIZOMSAIDIA MWALIMU

Sote tunaelewa kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa ni mtu mwenye kipaji cha aina yake. Alikuwa muelewa wa mambo katika mapana yake, mwenye kipaji cha juu cha kufikiri na mbunifu mkubwa. Pia alikuwa na uwezo mkubwa wa kujieleza na kuyachambua mambo mazito kwa lugha nyepesi ikiwa kwa Kiswahili na kiingereza.

Lakini pia ni muhimu kutambua kwamba asili ya nguvu zake ni watanzania na Chama Cha Mapinduzi. Umadhubuti na misimamo thabiti ya Chama Chama

Mapinduzi ndio vitu vilivvyomuwezesha baba wa Taifa kufanya mengi. Kwa hiyo, somo moja ambalo jamii yetu na hasa ninyi vijana wa CCM mnapaswa muelewe ni jinsi gani ya kuimarisha chama na kuhakikisha kwamba kinasimamia kikamilifu malengo yake, misingi yake na maadili yake.

**MWALIMU NA UONGOZI WA AWAMU ZILIZOFUATA.**

Viongozi wakuu wa taifa letu waliomfuatia Mwalimu, Rais wa awamu ya Pili Mzee Ally Hassan Mwinyi na Rais wa awamu ya Tatu Ndugu Benjamin William Mkapa wametoa mchango mkubwa katika kuendeleza baadhi ya mambo aliyosimamia Mwalimu Nyerere.

Pia ni dhahiri kwamba, Rais wa awamu ya Nne Dr Jakaya Mrisho Kikwete ametoa na anaendelea kutoa mchango muhimu katika kuyasimamia mambo muhimu ambayo Mwalimu aliyatilia mkazo kama vile Muungano wetu, Vita dhidi ya maadui Ujinga, Maradhi na Umasikini na pia kuendeleza mfumo wa demokrasia katika nchi yetu.

Kwa vile mtoaji mada atazungumzia mafanikio ya serikali ya CCM na hasa ya Serikali awamu ya Nne, sitakwenda kwa undani katika masuala hayo. Lakini ningependa kuzungumzia kwa kifupi masuala machache ambayo yalikuwa masuala muhimu kwa Mwalimu Nyerere ambayo naamini Rais Kikwete amesimama imara kuyaendeleza.

Mwalimu pamoja na Mzee Karume ndio waasisi wa Muungano wetu. Wote hawa waliamini katika umuhimu wa umoja na ushirikiano baina yetu. Walielewa kuwa muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni muungano wa nchi mbili huru. Muungano

wa nchi mbili sawa ambazo mazingira yake sio sawa katika mambo kama vile idadi ya watu na maeneo ya nchi. Kwa upeo huo walikubaliana juu ya mfumo na taratibu ambao kwa upande mmoja unalinda na kuimarisha muungano na kwa upande mwengine unakidhi mazingira maalumu ya muungano huo.

Suala la kudumisha Muungano wetu na hali ya kisiasa Zanzibar ni moja ya masuala muhimu ambayo Rais wa Awamu ya Nne Ndugu Kikwete ameweza kuyashughulikia kwa kwa uzito wake akielewa umuhimu na unyeti wake. Itakumbukwa kwamba katika mambo aliyoyapa kipaumbele mara tu baada ya kuchaguliwa ilikuwa ni suala hili la kuondosha uhasama Zanzibar.

Akihutubia bunge mwezi Desemba mwaka 2005, Rais wetu alizungumzia kwa uzito wake mpasuko wa kisiasa huko visiwani na umuhimu wa kutafuta ufumbuzi wa kudumu kwa kushirikiana na viongozi wa Zanzibar. Rais Kikwete kwa kofia zake zote mbili za Urais na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, akishirikiana kwa karibu na viongozi wa CCM na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, walichukua hatua ambazo hatimaye zilileta maridhiano kutokana na uongozi thabiti wa Rais wa Zanzibar Dr Aman Abeid Karume na Katibu Mkuu wa CUF Maalim Seif Sharif Hamad.

Na hapa ningelipenda kusisitiza kuwa mazungumzo haya yalikuwa ya muda mrefu ambayo yalishirikisha viongozi mbalimbali wa chama na serikali zote mbili, yaani serikali ya Jamhuri na Muungano na serikali wa Mapinduzi ya Zanzibar. Miongoni mwao alikuwepo Mzee Kingunge ambaye pamoja na wenzake wa pande zote mbili wajumbe wa kKmati Maalumu walijishughulisha sana na kupambana na changamoto nyingi hadi kufikia mahala mazungumzo yalipotufikisha. Suala hili lilijadiliwa hadi kufikia katika kikao cha Butiama ambapo mapendekezo yake yalikubaliwa na

Halmashauri Kuu ya Taifa. Lakini pia kuliamuliwa kuwepo na kura ya maoni. Jambo ambalo hapo mwanzo halikuafikiwa na ndugu zetu wa CUF lakini hatimaye maridhiano yakapatikana na kura ya maoni ikafanyika huko Zanzibar.

Katika kufuatilia suala hili, Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa namna moja au nyingine aliendeleza msimamo ambao alioweka Baba wa Taifa baada ya uchaguzi uliofanyika huko visiwani mwaka 1995. Mwalimu wakati ule, kutokana na hali ilivyokuwa huko visiwani humo, alishauri kuwepo na serikali ya umoja wa kitaifa.

**Ndugu Viongozi na Ndugu Wanakongamano;**

Mchango mwengine mkubwa alioutoa Mwalimu kwa taifa ni kusaidia kujenga misingi ya kidemokrasia pamoja na utaratibu wa viongozi wa kitaifa kubadilishana vijiti pindi muda unapowadia. Msingi ambao umekuwa ni sehemu ya utamaduni wetu na kuifanya nchi yetu kuonekana kama kielelezo cha mafanikio ya utamaduni huo barani Afrika. Mwalimu aliweza kujenga msingi madhubuti ambao ni tofauti na utamaduni uliokuwepo miongoni mwa viongozi wengi wa kiafrika ambao walijejengea fikira kuwa bila yao nchi haiwezi kwenda mbele.

Katika bara letu la Afrika bado wapo viongozi kadhaa ambao wanaendelea na imani hiyo potofu lakini kwa ujumla Mwalimu Nyerere alijenga msingi madhubuti unaotambua kwamba uongozi wa nchi ni lazima utegemee ridhaa ya watu. Daima aliamini kuwa nchi ni kubwa kuliko kiongozi fulani.

Rais wa awamu ya nne Ndugu Jakaya Kikwete ameweza na anaendelea kutoa mchango wake wa kuendeleza ujenzi wa misingi ya kidemokrasia. Rais Kikwete

ameweza kuandaa mazingira ambayo yameziwezesha asasi mbalimbali za nchi zikiwemo Mahakama na Bunge letu kukuza misingi ya demokrasia na utawala wa sheria. Ingawa bado kuna changamoto kadhaa za kushughulikia ni ukweli usiofichika kuwa asasi zetu hizi pamoja jumuiya za kiraia na vyombo vya habari vemeweza kupiga hatua katika kutekeleza wajibu wake kwa ujenzi wa taifa la kidemokrasia, lenye kuthamini umoja na mshikamano wetu na maslahi ya watanzania kwa ujumla.

**Ndugu viongozi na Ndugu Washiriki wa Kongamano,**

**MAJUKUMU YA VIJANA SASA NA BAADE:**

Vijana wetu hasa vijana wa Chama Cha Mapinduzi wana jukumu kubwa la kufuatilia na kujua historia ya Taifa letu. Vijana wanapaswa kutambua na kuthamini juhudi za wazee wetu ambao walijitolea kupigania uhuru wetu na kujenga taifa letu lakini pia kujitolea kusaidia kupigania uhuru, heshima na utu wa waafrika kwa jumla.

Vilevile vijana wanapaswa kuelewa mbinu zilinazotumika na wapinga maendeleo hasusan zile za kuwagawa watu ama nchi katika misingi ya ukabila, udini, uasili, maeneo, kijinsia na kadhalika. Ni jukumu la vijana wa Umoja wa Vijana wa CCM kuwa mfano wa kuigwa katika kuishi maisha yanayoendana na misingi ya utaifa wetu.

Amani na utulivu ni mambo ya msingi kabisa katika taifa lolote. Sisi watanzania tumebahatika kwamba nchi yetu kwa muda wote huu imekuwa ya utulivu, amani na ushirikino na nchi ya kipigiwa mfano. Lakini ni muhimu tutambue kuwa hali hii haikuja hivihivi tu. Imetokana na misingi thabiti iliyoandaliwa na baba wa taifa na viongozi wengine wasisi wa taifa letu.

Kwani kama jamii, watanzania hatutofautiani sana na ndugu zetu wengine katika bara la Afrika kama vile Burundi, Kongo, Rwanda, Somalia, Sudan na wengineo ambao nchi zao zilikumbwa ama zinaendelea kukumbwa na migogoro. Kilichotowezesha kuwa na tofauti na kuwa na utulivu na amani ni ile misingi inayojali utu, ushirikiano na mshikamano wa watanzania na dini, ukabila ama maeneo kutokuwa ni chanzo cha kuleta migogoro. Ukimuona yeyote ambaye anataka kubomoa misingi hiyo umuepuke kama ukoma.

Vijana wanapaswa kuwa na utashi na ushawishi wa kujua masuala mbalimbali yanayolikabili taifa letu lakini pia masuala na changamoto mbalimbali zinazolikabili bara letu na dunia kwa ujumla. Mwalimu Nyerere alikuwa muumini mkubwa wa kujiendeleza kielemu na kimaarifa. Daima aliamini kwamba watu wanapaswa kujua.

Ni jukumu la vijana wa CCM kuwa mfano wa kuigwa katika ujenzi wa taifa lenye kuthamini utu na haki ya kila mmoja wetu huku wakiendeleza juhudi za ujenzi wa mfumo wa kidemokrasia ambao Mwalimu Nyerere aliupigania na kuusimamia katika maisha yake, iwe wakati wa demokrasia ya chama kimoja ama wakati wa vuguvugu la demokrasia ya vyama vingi. Na hili litafanikiwa endapo vijana wa CCM watakuwa ndio kioo cha uthibitisho wa jinsi gani watanzania wanathamini utamaduni wa kutatua tofauti zao za kisiasa, kijamii na kimaendeleo bila ya kugombana ama kutoleana matusi. Vijana wetu mnapaswa kuwa mahiri katika kutumia nguvu ya hoja na sio hoja za nguvu katika kuhakikisha kuwa tunaendeleza, tunalinda na tunatetea demokrasia yetu inayofuata misingi ya utaifa wetu.

Ni jukumu la vijana ambao ndio viongozi wa sasa na baadaye kuhakikisha kuwa wakati tunajitahidi kuendana na mahitaji ya sasa na mabadiliko ya mazingira ya

kiuchumi duniani, Chama chetu kinaendelea kuwa mstari wa mbele wa kuhakikisha kuwa tofauti kati ya walio nacho na wasio nacho haikui kiasi cha kuhatarisha usalama na umoja wa taifa letu. Haya yanaweza yakafanyika hata kwa kufuata mfumo wa soko huria lakini ule ambao unajali maslahi ya Mtanzania kwanza wakati ukitambua umuhimu wa ushiriki wa marafiki na wawekezaji wa nje.

Kufanya hivi ni kumuenzi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alitambua kuwa dunia inabadilika na hapana budi isipokuwa kuongoza mapambano ya kuleta mageuzi nchini mwetu huku tukiendelea kupigania kujenga taifa lenye umoja, amani, utulivu na mshikamano na lenye kuzingatia maslahi ya wananchi kwa jumla.

**Asanteni kwa kunisikiliza**